# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SEREKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA

## MTIHANI WA HALMASHAURI WA UTIMILIFU

## KIDATO CHA NNE

**MSIMBO: 015** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

**MUDA: SAA 3: 00** **2025**

UB

**MAELEKEZO**

Karatasi hii ina sehemu A,B na C Zenye Jumla ya Maswali kumi na moja (11).

Jibu Maswali yote katika sehemu A,B na maswali mawili tu ( 2 ) kutoka sehemu C.

Sehemu A ina alama kumi na sita ( 16 ),sehemu B ina alama Hamsini na nne (54 ) na sehemu C ina alama thelathini ( 30).

Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali

Simu za mkononi na vitu vyote visivyo husika havitakiwi katika chumba cha mtihani.

www.ujuziblog.com

**SEHEMU A (ALAMA 16 )**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Katika kipengele cha (i)-(x) chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika karatasi yako ya kujibia

(i) kwa kuzingatia mafundisho ya uislamu,bainisha njia za kumjua Mwenyezi Mungu (s.w)

A. Wahyi,mazingira na ilhamu

B. fitra,nafsi ya mwanaadamu na wahyi

C. vipaji,fitra na umbile la mbingu

D. Wahyi,nafsi na umbile la ardhi.

(ii) Jambo gani halikufanywa na mtume (s.a.w) katika mchakato wa kuhifadhi qur'an?

A. kuwaamrisha maswahaba kujifunza qur'an

B. kuhifadhiwa kwa kusomwa mara kwa mara

C. qur'an kutumika katika ibada ya swala

D. kuchagua wahariri wa qu'an tukufu.

(iii) Imamu Malik bin Anas ni mwandishi mashuhuri wa hadithi aliyejitokeza katika kipindi kipi?

A. Tabii Tabiin

B. maswahaba

C. mtume (s.a.w)

D. Tabiin

E. makhalifa

(iv) Sunnah za mtume (S.A.W) ni muhimu kufuatwa na muislamu kwa sababu

A. Muislamu anaweza kuwa nabii baadae

B. Huwezi kutekeleza Qur_an bila ya kufuata sunna

C. Ukiacha sunnah utapata dhambi

D. Sunnah ni sehemu ya Qur-anm.

(v) Ni aina gani ya Tawaf ambayo huambatana na matendo ya nguzo za Hija na hujulikana kamaTawaful-Ziyaara

A. Tawaful- Widaa

B. Tawaful-Quduum

C. Tawaful-Ifadha

D. Hija ya Qiraani

(vi) Mja anapotaka kuingia katika Uislamu anatakiwa kuchukua ahadi ya utii.Bainisha ahadi hiyo kati ya hizi zifuatazo.

A. Kuishi kwa kufuata barabara sunnah

B. Kuishi kwa mujibu wa kitabu na Sunnah

C. Kuishi kwa kutekeleza swala tano na funga

D. Kuishi kwa kufuata barabara Qur'an.

www.ujuziblog.com

(vii) Ni Mzozo gani uliotatuliwa kwa kutumia hadithi za mtume (s.a.w)

A. Swahaba gani atakuwa kiongozi baada ya kufariki Mtume (s.a.w)

B. Adhabu kwa walio kataa kutoa zakat baada ya kufariki Mtume (s.a.w)

C. Idadi ya miaka ambayo kiongozi wa dini ya kiislamu ataongoza

D. Sehemu ambayo Mtume (s.a.w )atazikwa baada ya kufariki

(viii) Suratul mauun inatoa mafunzo mengi muhimu kwa waislamu ispokuwa

A. kuwafanyia wema mayatima

B. kuwahurumia maskini

C. kuepuka ria

D. Kutopuuza swala

E. kuwatii wazazi na walezi.

(ix) Lipi ni lengo la kuamrishwa waislamu kusimamisha nguzo tano za uislamu

A. Kuzielewa ibada maalumu

B. Kufanya Ummah huu kuwa bora na ulio teuliwa na Allah (s.w)

C. Ili kumjua Allah ((s.w) na kumtukuza katika ibada

D. Kuwa Khalifa na kusimamisha dola popote ulimwenguni

(x) Katika kukubaliwa au kukataliwa kwa wanazuoni wamezigawanya hadithi katika makundi gani?

A. Hadithi sahihi, Hadithi Hassan, Hadithi Dhaifu na Hadithi Maudhu

B. Hadithi Hassan, Hadithi Dhaifu na Matini

C. Sanadi, Matini na Rawi.

D. Hadithi Qudussiyi na Hadithi Hassan

2. Oanisha kifungu cha maneno kutoka Orodha **A** na kile cha Orodha **B** Kisha andika herufi ya jibu lake kwenye jedwali.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| (i) Basi sali kwa ajili ya Mola wako na uchinje kwa ajili ya mola wako )Nakila utakalolifanya lifanye kwa ajili ya Mola wako, siyo mizimu wala mapango wala makaburi | A. Sunnah za swala |
| (ii) Kusoma takbirah,tahmiid na dua katika rukuu,itidali na sijda. | B. Kusimamisha swala |
| (iii) Kuzikusanya swala mbili katika wakati swala ya mwanzo | C. Nguzo za swala |
| (iv) Kumkinga mja na mambo maovu na machafu | D. Faradhi Ain |
| (v) Sunnah inayoswaliwa baada ya kuchomoza jua na kabla ya mchana | E. Dhuhaa |
| (vi) Ruhusa za kutayammamu kwa muislamu | F. Jamu’u Taakhir |
| | G. Ugonjwa usioruhusu kutumia maji |
| | H. Swala |
| | I. Jamu’u Taqdiim |
| | J. Faradhi kifaya |

**SEHEMU B (Alama 54)**

**Jibu maswali yote kwa ufupi sehemu hii**

3. a)Uislamu umezigawa haki za mwenyezi mungu katika sehemu mbili. Taja haki hizo

   b) Mtume Muhammadi(s.a.w)aliandaliwa kwa njia ya ilhamu kabla ya kupewa utume. Bainisha mambo matatu yanayoonesha kuwa Muhammadi alikuwa katika makuzi yaliyo simamiwa na M/mungu(s.w )
4. Kwa kuzingatia kuchaguliwa kwa Abubakar(r.a) kuwa khalifa wa kwanza wa dola ya kiislamu baada ya kutawafu mtume (s.a.w),eleza sifa tatu za kiongozi.
5. Eleza mambo manne ambayo Mwenyezi mungu (s.w) ameitofautisha qur'an na vitabu vingine vilivyopita.
6. a) Nini maana ya Sai

   b) Toa mafunzo matatu anayopata muislamu kutokana na kitendo cha sai katika ibada ya Hija
7. Muumini ni Yule anaye leta toba ya kweli atakapo teleza na kumuasi mola wake .Taja sharti nne za toba ya kweli

8 . a) Unafahamu nini kutokana na neno "Imani"

b) Sema " Bila shaka wa kwanza na wa mwisho wote watakusanywa kwa wakati uliowekwa. katika siku maalumu" (56:49-50) .Kutokana na aya hii, siku ya mwisho lazima iwepo.Thibitisha kwa hojo nne(4) kuonesha ulazima wa siku hiyo.

**SEHEMU C (Alama 30)**

**Jibu maswali mawili tu katika sehemu hii kwa njia ya insha**

9. Bainisha vikwazo sita katika kutekeleza ibada ya zakat kwa jamii ya waislamu wa Tanzania.

10. Waislamu walio wengi hushindwa kuwaswalia ndugu zao waislamu wanapo fariki. Ukiwa wewe umepata Elimu hiyo. Elezea namna utakavyo tekeleza swala ya maiti kwa kufuata taratibu za swala hiyo.

11.Baadhi ya watu katika jamii wanachukia ndoa za wake wawili hadi wanne.Kwa kutumia hoja nne(4) waelimishe watu hao kwa kuonesha ndoa hizo ni rehema kwa watu wote duniani.

UB